Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...

Napenda kuungana na walionitangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa kibali cha kukutana mahali hapa kwa ajili ya tamasha hili la Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA. Nawaletea salamu nyingi za upendo kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais, anawatakia mashindano mema na amenituma niwaeleze kuwa ataendelea kuboresha miundombinu ya michezo nchini ili kuhakikisha Taifa linakuwa na wanamichezo mahiri wanaoweza kuwakilisha Tanzania ndani na nje ya nchi.

Nichukue fursa hii pia kukushukuru Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb.), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mashindano haya. Nafahamu ufunguzi ulitakiwa ufanyike tarehe 3 Juni lakini ilishindikana kutokana na majukumu niliyokuwa nayo, hivyo ililazimu kusogeza mbele hadi leo tarehe 6 Juni ili kuniwezesha kuungana nanyi, nawashukuru sana!

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Viongozi na Wananchi wote wa Mkoa wa Tabora kwa kazi kubwa na nzuri ya maandalizi na kuweka mazingira salama kwa ajili ya watoto wetu kushiriki kikamilifu katika mashindano haya. Hali kadhalika, napenda kuwapongeza Walimu pamoja na wazazi/walezi kwa kuwaandaa vizuri wanamichezo hawa tangu ngazi ya Shule/Skuli, Kata, Halmashauri, Mkoa na sasa Taifa. Nimefurahi pia kuona ushiriki wa wanafunzi kutoka Zanzibar katika mashindano haya. Kitendo hiki siyo tu kinaimarisha na kudumisha Muungano wetu bali kinajenga utamaduni mzuri wa mashirikiano baina yetu. **Hongereni sana!**

Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wanamichezo na Wananchi wote,

Serikali inatambua kuwa maandalizi ya wachezaji mahiri hayana budi kuanza katika umri mdogo na kuwa endelevu. Na hii ndio sababu ya kuwepo kwa mashindano haya ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA ili kusaidia kuibua mapema vipaji vipya na kuviendeleza. Kwa kutambua hilo, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, tangu aingie madarakani ameendelea kutoa hamasa kwa wanamichezo wetu na kuhakikisha sekta ya michezo inapata fedha za kutosha, na tayari matunda yameanza kuonekana. Nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa

Rais kwa kupatiwa tuzo kutoka Baraza la Michezo la Taifa kutambua mchango wake mkubwa katika maendeleo ya michezo nchini tarehe 17 Machi, 2023.

Aidha, nichukue fursa hii kuzipongeza shule za Serikali zilizoonyesha uwezo wao mkubwa kwa kufanya vizuri katika mashindano ya michezo mbalimbali. Shule hizo ni (i) Shule ya Sekondari Kilombero ya Mkoa wa Morogoro iliyoshiriki na kuwa mabingwa wa mashindano ya Kanda ya Tano kwa mchezo wa mpira wa mikono kwa vijana wenye umri wa chini ya miaka 17 mwaka 2023; (ii) Shule ya Msingi Mkalapa Wasichana kutoka mkoani Mtwara waliokuwa mabingwa wa mchezo wa wavu katika mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Mkoani Arusha Septemba 2022; na (iii) Shule ya Msingi Benjamin Mkapa ya Jijini Dar es Salaam iliyoshiriki mashindano ya mpira wa miguu Ukanda wa CECAF yaliyofanyika nchini mwezi Disemba 2022. Ninazisihi shule nyingine ziige mfano huu wa shule hizi nilizozitaja katika michezo mbalimbali.

Waheshimiwa Viongozi na Wanamichezo,

Kaulimbiu ya mashindano ya mwaka huu inasema ***"Uimarishaji wa Miundombinu ya Shule Nchini uwe Chachu ya Maendeleo ya Taaluma, Sanaa na Michezo"***. Kaulimbiu hii inasadifu kazi kubwa inayofanywa na Serikali katika kuboresha miundombinu katika sekta ya Elimu. Kupitia miradi ya BOOST, SEQUIP, EP4R na LANES, Serikali Kuu imetoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya, madarasa, maabara, mabweni, nyumba za walimu, matundu ya vyoo pamoja na ukarabati wa miundombinu ya shule zilizochakaa katika Halmashauri zote nchini.

Aidha, kama Mheshimiwa Waziri - TAMISEMI alivyoeleza, Serikali inaendelea na mpango wa kuboresha miundombinu ya michezo katika Shule Teule 56 nchini. Hivi sasa tumekamilisha uboreshaji wa miundombinu ya michezo katika Shule za Sekondari Tabora Boys na Tabora Girls, na tuko kwenye maandalizi ya kuboresha shule nyingine Sita kwa kujenga viwanja vya Nyasi Bandia katika shule hizo, kwa gharama ya Shilingi Bilioni 24. Mradi huu utaanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18. Ukamilishaji wa miundombinu hii utawezesha wanafunzi kucheza katika viwanja vyenye viwango bora na kuwezesha maandalizi ya wanamichezo mahiri. Hivyo, nawaagiza Viongozi wa Mikoa na Halmashauri husika kusimamia kwa uadilifu na uaminifu miradi hii ili ikamilike kwa wakati na iendane na thamani ya fedha. Chukueni hatua za haraka pale unapotokea ubadhirifu au kasoro zozote. Kiu ya Serikali ni kuona nchi inakuwa na wanamichezo mashuhuri duniani watakaoitangaza vema Tanzania,

watakaoweza kuinua maisha yao kiuchumi pamoja na kuchangia katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Aidha, nitumie fursa hii pia kutoa msisitizo wa kipekee katika kukuza michezo kwa ndugu zetu wenye ulemavu wa viungo (Paralympic Games). Aina hii ya michezo siyo tu inasaidia kuboresha afya za ndugu zetu wenye ulemavu wa viungo bali inasaidia kukuza vipaji vyao na kuliwezesha kundi hilo maalum kutimiza ndoto zao za kushiriki katika mashindano ya michezo ya walemavu.

Waheshimiwa Viongozi na Wanamichezo,

Ili kufanikisha mikakati iliyopo ya kuboresha michezo na taaluma nchini, hakuna budi kuhakikisha na kuzingatia yafuatayo:

Moja, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhakikisha kila shule ya Msingi na Sekondari ina Mwalimu wa michezo walau mmoja. Hii itasaidia kuimarisha michezo shuleni, kuwezesha somo la michezo kufundishwa kitaalamu na pia kuhakikisha linafundishwa bila kukosa. Vilevile, hakikisheni Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo yanalindwa, msibadilishe matumizi. Kumekuwa na utaratibu wa kutumia maeneo ya michezo kujenga madarasa, maabara na vyoo kwenye shule zetu hasa maeneo ya Mijini. Utaratibu huu haukubaliki. Wasimamizi wa elimu hakikisheni shule mpya zinazojengwa zinakuwa na maeneo ya kutosha kwa ajili ya viwanja vya michezo. Aidha, Uboreshaji wa miundombinu ya shule kwa ajili ya michezo uendane na suala zima la usafi na uhifadhi wa mazingira. Nasisitiza upandaji miti kuzunguka viwanja vya michezo ili kuhakikisha upatikanaji wa hewa safi wakati vijana wanapofanya mazoezi au kushiriki mashindano mbalimbali.

Pili, Ratiba ya michezo shuleni izingatiwe. Kumekuwa na utaratibu katika baadhi ya shule kutozingatia ratiba ya michezo na badala yake kutumia muda wa kipindi cha michezo kufundisha masomo mengine. Jambo hili si sawa. Ni lazima kuwapa wanafunzi muda stahiki kushiriki katika michezo ili kuibua na kuendeleza vipaji vyao. Hivyo, nawataka Wasimamizi wa Elimu katika ngazi zote nchini kuhakikisha suala hili linazingatiwa;

Tatu, Wizara ya Michezo angalieni namna ya kushirikiana na wadau wengine wa michezo kubuni na kuandaa mipango ya kuwaendeleza vijana wenye vipaji katika michezo na pia kuwapa motisha wanafunzi wanaoshiriki na kufanya vizuri

katika michezo. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashiriki kwa kushirikiana na Wizara ya Michezo, tafuteni fursa mbalimbali za ufadhili ili kuwezesha wanafunzi wetu kubadilishana uzoefu (*exchange programs*) na kunolewa zaidi katika vilabu mashuhuri vya michezo duniani au kutoka kwa wataalamu wa kimataifa katika fani mbalimbali za michezo.

Nne, natoa pongezi kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa hatua madhubuti mnazochukua ili kutatua baadhi ya changamoto katika sekta ya elimu, michezo na sanaa. Lakini pamoja na jitihadi hizi, kuna haja ya kuchukua hatua za makusudi kuongeza usimamizi wa utoaji wa elimu utakaowezesha kujenga stadi na umahiri katika masomo na katika kuimarisha maadili kwa watoto wetu. Hivi karibuni, tumeshuhudia mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu. Hivyo, shirikianeni na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuweka msisitizo kwenye maadili katika mifumo yetu ya elimu ili tuandae wahitimu watakaokuwa waadilifu, wanaojali na kuheshimu utu, mila na desturi za kitanzania;

Tano, nafahamu kuna baadhi ya shule na taasisi binafsi ambazo zinafanya vizuri katika michezo na wameenda mbali zaidi kwa kuwa na klabu za michezo na kuratibu ushiriki wa vijana wetu katika mashindano mbalimbali nje na ndani ya nchi. Napenda kutumia nafasi hii kuzipongeza sana shule hizo mojawapo ikiwa ni *Shule ya Msingi na Sekondari ya Fountain Gate ya Dodoma* kwa ubunifu ambao umesaidia kukuza vipaji vya watoto wetu na kuwawezesha kushiriki na kushinda katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tambueni mambo haya mazuri yanawezekana pia hata katika shule zetu za Serikali. Nendeni mkajipange na kuweka utaratibu mzuri kwa kuiga mfano huo.

Sita, nawapongeza vijana wetu wa Shule ya Sekondari ya Kisimiri kwa kuonesha uwezo mkubwa na ukakamavu katika kutuburudisha kwa Brass Band. Naomba tuwapongeze sana watoto wetu hawa pamoja na walimu wao kwa kurejesha utaratibu ambao shule zote zilikuwa na Brass Band ya Shule miaka ya nyuma. Sasa nazitaka shule zote kuwa na utaratibu wa kuwajengea ukakamavu vijana wetu.

Saba, ninaielekeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Chama cha Wanariadha Tanzania, Chama cha Walemavu na sekta binafsi kuweka nguvu pamoja katika kuinua michezo ya riadha na ya walemavu

ambayo imeonekana kuwa na tija kubwa kwa Taifa lakini haipewi uzito inaostahili.

Ndugu Wanamichezo na Wananchi wote,

Serikali itaendelea kuboresha mashindano haya na kuyafanya kuwa kisima cha wanamichezo mahiri wa Taifa letu. Aidha, nawapongeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kuandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashindano haya ambao nitauzindua rasmi leo. Hili ni jambo zuri katika kuhakikisha mashindano haya yanaandaliwa kwa ubora wa hali ya juu. Napenda kuwahakikishia kuwa, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kuunga mkono wanamichezo wetu na kuzipa kipaumbele sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ili ziweze kufaidisha vijana wengi zaidi. Aidha, kupitia michezo hii, serikali itaendelea kutoa fursa kwa wanamichezo wanaofanya vizuri zaidi kushiriki katika mashindano ya kimataifa ili kuendelea kuwajengea uzoefu zaidi. Hivyo, napenda kutumia nafasi hii kuwatia moyo na kuwahakikishia kuwa sekta hii ya michezo itazidi kuimarika na kutengeneza nafasi zaidi ya ninyi kufanikisha ndoto zenu. **Changamkieni fursa!**

Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wanamichezo na Wananchi wote,

Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuhimiza jamii ya Watanzania kutambua na kuthamini michezo na sanaa, pia kusaidia na kuwatia moyo watoto wetu wenye ndoto za kufanikiwa kupitia vipaji vyao. Sekta ya michezo ni uchumi na pia ina nafasi ya kuajiri vijana wengi na kutengeneza matajiri wengi endapo vipaji vya vijana wetu vitaendelezwa. Vilevile, michezo inasaidia sana katika kuitangaza nchi yetu na lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Kamwe tusiwe vikwazo kwa vijana wetu kufikia ndoto zao. Kadhalika, napenda kuwahimiza wananchi kujenga tabia ya kufanya mazoezi mara kwa mara. Tusisubiri maelekezo ya madaktari ili kufanya mazoezi. Tujitahidi kushiriki michezo au kufanya mazoezi ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mwisho, ninaamini kuwa wanafunzi wetu mmejiandaa vizuri kushiriki na kushinda makombe na medali katika mashindano haya. Kwa maandalizi yaliyofanywa ninaamini mtashindana kwa usawa na haki pasipo kuhasimiana na hatimaye washindi kupatikana. Nawatakia mashindano mema na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema, kwa kipindi chote cha mashindano haya na kuwawezesha kurejea nyumbani salama. Nimeelezwa kuwa, mashindano haya yatatumika pia kuwapata wawakilishi wa nchi yetu katika mashindano ya Afrika Mashariki, ambayo kwa mwaka huu 2023 yatafanyika mwezi Agosti, nchini

Rwanda. Natanguliza pongezi kwa wale wote watakaochaguliwa kuliwakilisha Taifa katika michezo hiyo na kuwatakia kila la kheri katika safari yao.

Baada ya kusema haya, sasa natamka rasmi kuwa Mashindano ya Michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa mwaka 2023 yamefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza!